# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA NNE

**11 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 11 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 05 la tarehe 31 Januari, 2025;
2. Toleo Na. 06 la tarehe 07 Februari, 2025;
3. Toleo Na. 07 la tarehe 14 Februari, 2025;
4. Toleo Na. 08 la tarehe 21 Februari, 2025;
5. Toleo Na. 09 la tarehe 28 Februari, 2025;
6. Toleo Na. 10 la tarehe 07 Machi, 2025;
7. Toleo Na. 11 la tarehe 14 Machi, 2025
8. Toleo Na. 12 la tarehe 21 Machi, 2025;
9. Toleo Na. 13 la tarehe 28 Machi, 2025; na
10. Toleo Na. 14 la tarehe 04 Aprili, 2025.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**41. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati wa Shule za Msingi chakavu za Mtimbola, Mhulidede, Kigwa A, Itobela, Kalola, Igoko, Imalauduki na Ikongolo - Uyui.

**42. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza umri kwa Vijana wa Kiume wanaopata mikopo ya Halmashauri kufikia miaka 50.

**43. MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

**44. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaunga mkono juhudi za Wananchi kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya Lupigi, Lufilyo, Kisegese, Lusafi na Kambasegele - Busokelo.

## WIZARA YA NISHATI:

**45. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha kupeleka umeme kwenye Shule na Taasisi zote zikiwepo za dini katika Mkoa wa Lindi.

**46. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Vijiji 42 vilivyobaki vya Wilaya ya Kishapu vitapatiwa umeme.

## WIZARA YA FEDHA:

**47. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Madarasa ya Elimu kwa Mlipa Kodi kupitia Vikundi vya Wanawake Wajasiriamali.

## WIZARA YA AFYA:

**48. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoani Rukwa.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**49. MHESHIMIWA MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB (DIMANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini JWTZ litafanya uhakiki na kuwalipa fidia Wananchi 13 waliobaki katika eneo la Kambi ya Jeshi Kisakasaka Zanzibar.

**WIZARA YA UJENZI:**

**50. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Godegode ikizingatiwa kuwa Mkandarasi ameshapatikana.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**51. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kuhamasisha Watanzania kutembelea Hifadhi na kuongeza mapato ya utalii badala ya kutegemea Watalii toka nje ya nchi.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**52. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itaboresha usikivu wa Radio ya TBC katika Mji wa Itigi.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**53. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kutoa huduma stahiki kwa Wafungwa Wajawazito.

**WIZARA YA KILIMO:**

**54. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Miradi ya Umwagiliaji iliyopo Jimbo la Kalenga inaleta tija kwa Wananchi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **11 APRILI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |